# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 10 Juni, 2019

*(Bunge Lilianza Saa 3.00 Asubuhi)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge karibuni tena tunaendelea na Mkutano wetu wa 15, leo ni Kikao cha 42.

Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Mhesimiwa Waziri Mkuu, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq.

Na. 345

### Wimbi la Vijana Kukimbilia Mijini

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** Aliuliza:-

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 inaonesha kwamba asilimia saba ya Watanzania wanaishi vijijini lakini katika miaka ya hivi karibuni watu wengi hasa vijana, wanakimbilia mijini wakidai kuwa maisha ni magumu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza au kudhibiti hali hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 asilimia 70.4 ya Watanzania wanaishi vijijini. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020 imeelekeza Serikali kuboresha na kukuza uchumi wa vijijini ili kuongeza tija ya uzaliashaji mali na kukuza uchumi katika maeneo hayo kwa lengo la kuongeza fursa zaidi za ajira kwa vijana. Katika kupunguza hali hii Serikali inatekeleza mipango ifuatayo:-

(i) Kuboresha miundombinu ya kiuchumi pamoja na huduma za jamii ikiwemo ujenzi wa barabara za vijijini, ili kuwezesha wananchi waishio vijijini kusafirisha malighafi, hasa mazao, kupeleka sehemu zenye masoko, Mpango wa Umeme Vijijini kupitia *REA,* ujenzi wa miradi mikubwa inayotoa fursa za ajira kwa vijana kama miradi ya ujenzi wa reli, mradi wa uzalishaji umeme *Stiegler's Gorge* na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za ugani.

(ii) Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa *SACCOS* za vijana zilizoundwa katika Halmashauri ili kujenga mitaji yao kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na mifuko mingine ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambapo katika mwaka 2017/2018 kiasi cha shilingi 783,280,000 kimetolewa kwa vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

(iii) Kutekeleza programu ya ukuzaji ujuzi nchini kwa lengo la kuwapatia vijana ujuzi utakaowawezesha kujiajiri, hususan vijijini. Mafunzo haya ni pamoja na mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya uanagenzi na urasimishaji wa ujuzi unaopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu ambapo katika mwaka 2018/2019 jumla ya vijana 32,563 wamewezeshwa kupata mafunzo hayo katika fani mbalimbali.

(iv) Ni kuandaa na kutekeleza mkakati wa Kitaifa wa kuwezesha vijana kushiriki katika kilimo, hususan vijijini. Mkakati huu unalenga kuwawezesha vijana wa ngazi mbalimbali za elimu kushiriki kikamilifu katika kilimo na hivyo kuongeza fursa za vijana kupitia sekta ya kilimo vijijini.

Katika kutekeleza mkakati huu Serikali inaendesha mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa teknolojia ya kitalu nyumba kwa vijana na takribani vijana 18,800 wamepata mafunzo hayo katika Halmashauri zote.

(v) Kusimamia utekelezaji wa Azimio la Wakuu wa Mikoa mwezi Novemba, 2014 lililotoa maelekezo ya kila Halmashauri nchini kutenga maeneo ya vijana na kuyatumia kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na biashara katika kila Halmashauri nchini.

(vi) Kutoa fursa za upendeleo kwa vikundi vya vijana wakiwemo wahitimu na wenye ulemavu ili kuwawezesha kupata fursa ya zabuni za Serikali kupitia sheria ya ununuzi wa umma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq nilikuona.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuanzisha programu mbalimbali lakini bado kuna tatizo la masoko. Je, Serikali ina mkakati gani sasa kuwasaidia vijana hawa katika upatikanaji wa masoko?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, vijana 32,563 waliopata mafunzo idadi yao ni ndogo sana ukilinganisha na vijana ambao wako maeneo mbalimbali vijijini.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuongeza idadi ya vijana wengi zaidi, walau waweze kufikia hata asilimia 50 ili kusudi waweze kuacha kukimbilia mijini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu kwa vijana wa Tanzania, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, nikianza na la kwanza kuhusu masoko; moja kati ya mpango ambao tunautekeleza ni mpango wa kuwashirikisha vijana kwenye kilimo ambao tunaufanya kwa pamoja na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa vijana wanaofanya shughuli za kilimo hivi sasa kupitia maelekezo ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi ambayo na mimi pia nimeshushiwa kwa ajili ya kuyatekeleza, hivi sasa tumeanzisha programu maalum ya kuanza kutafuta masoko ya bidhaa hasa bidhaa za kilimo za vijana wetu ambao wanafanya shughuli hizo kupitia viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunatarajia kwenda kutengeneza shamba kubwa la mfano katika eneo la Mboga, Wilaya ya Bagamoyo ambapo kipo Kiwanda cha Sayona ambacho kimekubali kununua matunda kutoka kwa vikundi vya vijana ambao sisi tutawatayarishia mashamba, lakini vilevile pamoja na kuwatafutia mbegu pamoja na Wataalam wa *SUA* wameshafika katika eneo hilo. Kwa hiyo, katika upande wa kilimo tumeanza kuzungumza na viwanda na makampuni makubwa, ili pia iwe sehemu ya soko kwa bidhaa za vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa wale vijana ambao ni mafundi, wameunda makampuni, wanafanya shughuli mbalimbali za utoaji huduma, hivi sasa yalitoka maelekezo kwamba, kila Halmashauri nchi nzima itenge asilimia kadhaa

ya manunuzi yake ya ndani kwa ajili ya vikundi hivi vya vijana. Na ninavyozungumza hivi vijana wengi wanaofanya shughuli za ufundi seremala ambao wanatengeneza madawati walipata kazi Halmashauri nyingi nchini kusambaza madawati, ikiwa pia ni sehemu ya soko, lakini pia kama Serikali tunaweka mpango mkakati mzuri kuhakikisha kwamba tunaweka mfumo endelevu wa vijana hawa kupata masoko ya uhakika. Hayo ni maeneo mawili tu ambayo nimeyatolea mfano.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ilikuwa ni kuhusu idadi ndogo ya vijana. Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza Programu ya Ukuzaji Ujuzi nchini ambayo imeanza mwaka 2016 mpaka mwaka 2021 yenye lengo la kuwafikia takribani vijana milioni nne ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, nilichokisema hapa ni *component* moja tu katika utekelezaji wa mradi huu, lakini tunawafikia vijana wengi na lengo letu ni kuwafikia vijana zaidi ya milioni nne ifikapo mwaka 2021.

Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tunafahamu vijana ni kundi kubwa, tunaendelea kuwafikia kwa kupitia programu mbalimbai, ili wote waweze kunufaika na urasimishaji ujuzi huo.

**SPIKA:** Naomba swali fupi, Mheshimiwa Rashid Shangazi na majibu yawe mafupi pia.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru sana kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa, kule Lushoto sisi tayari tumeshajiandaa na tuko tayari tunavuna matunda mengi sana, lakini masoko yake kwa kweli sio mazuri kiasi kwamba yanashawishi vijana kuachana na kilimo cha matunda na kwenda mjini.

Je, Serikali ina mkakati gani kusaidia kutupatia masoko ya uhakika wakulima wa matunda kule Lushoto?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, masoko ya wakulima vijana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namba ambavyo anawapigania vijana katika eneo lake na niseme tu kwamba katika majibu yangu ya awali niliyoyasema eneo mojawapo ambalo pia tutalifikia ni eneo la Lushoto lenye matunda mengi sana na tayari tumeshaanza mazungumzo na mwekezaji mkubwa kabisa Ndugu Bakhresa kwa ajili pia ya kuona namna ambavyo tunaweza tukasaidiana naye tukapata mahitaji ya matunda ambayo anayahitaji kule kiwandani, ili vijana wa Lushoto kupitia utaratibu ambao tumeuweka tuwawezeshe waweze kulima na baadae soko liwe ni kupitia Ndugu Bakhresa na kampuni nyingine za vinywaji hapa nchini.

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata, nalo linaelekea TAMISEMI la Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi. Mheshimiwa Masaburi tafadhali uliza swali lako.

Na. 346

**Kutenga Maeneo Maalum ya Kufugia Samaki**

**MHE. JANETH M. MASABURI** Aliuliza:-

Nchi yetu imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi zikiwemo bahari, maziwa, mito na mabwawa mengi ya asili pamoja na rasilimali watu kubwa ambao hawana ajira.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vijana na akina mama kwenye kila Halmashauri nchini kutenga maeneo maalum ya kujenga mabwawa ya kufugia samaki ili makundi hayo yapate kujiajiri?

**SPIKA:** Majibu ya swli hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili Halmashauri zote nchini zimeelekezwa kutenga maeneo ya ardhi kwa ajili ya kuchimba mabwawa ya kufugia samaki, kuendeleza ufugaji wa samaki kwenye vizimba na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali kwa ajili ya uzalishaji bora na endelevu wa samaki.

Mheshimiwa Spika, jitihada zetu nyingine za Serikali za kuwasaidia wavuvi nchini wakiwemo vijana na akinamama ni kuondoa kodi katika zana za malighafi yaani uvuvi kwa *engine* za kuvulia, nyavu, kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani yaani *VAT* kwenye *engine* za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu na vifungashio ili kupunguza gharama za zana na vyombo vya uvuvi na kutoa ruzuku kwenye zana za uvuvi ambapo mvuvi anatakiwa kuchangia asilimia 60 na Serikali ni asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote nchini zimekuwa zikipewa mafunzo ya uvuvi endelevu kwa wavuvi wakiwemo vijana na akinamama kupitia semina, warsha, vipeperushi, makala, redio na luninga kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wadau mbalimbali. Pia Maafisa Uvuvi katika Halmashauri zote nchini wamepatiwa mwongozo wa ugani katika sekta ya uvuvi kwa lengo la kutoa elimu kwa wavuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji na kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambapo jumla ya nakala 1,000 zilisambazwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masaburi nimekuona.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza TAMISEMI kupitia Mawaziri wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya hapa nchini. Tumekuwa tukiwaona wanatekeleza wajibu wao ipasavyo, lakini katika eneo hili la vijana na wanawake ninaomba niulize maswali kama yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wengi na wanawake hapa nchini wameshindwa kufanya biashara zao kwa tija kutokana na ukosefu wa ujuzi na maarifa wa kufanya biashara hizo. Je, Serikali iko tayari kuiwezesha kutoa mafunzo makundi haya ya ufugaji wa samaki ya uhakika na kwa idadi kubwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa, sekta ya uvuvi imeonesha kuwa na fursa kubwa ya kukuza ajira, kukuza kipato, kuboresha lishe na hata kuiingizia Serikali fedha za kigeni. Je, Serikali iko tayari kuanzisha mpango wa kujenga vizimba pembezoni mwa maziwa na mabwawa na hata kandokando ya mwambao wa bahari?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, tafadhali. Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa pongezi ambazo ametutumia kwenye Ofisi ya TAMISEMI kwa kazi ambayo inafanyika tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Masaburi ametoa maswali mawili, swali la kwanza anatuhimiza tuwe na mafunzo kwa vijana na akinamama na kweli hili jambo linafanyika, kwa sababu jambo la msingi ni kwamba tumeshatoa maelekezo kila Halmashauri ina maelekezo na baada ya kugundua kwamba kuna ... pia na mafunzo ... mtaji ndio maana Bunge hili tukufu likapitisha sheria kwamba kila Halmashauri itatenga mapato yake ya ndani asilimia nne kwa akinamama, nne kwa vijana na mbili kwa watu wenye

mahitaji maalum au wenye ulemavu kwa hiyo hii pia ni sehemu ya mtaji.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kila Halmashauri ina Maafisa wa Ustawi wa Jamii na kuna Maafisa wa Vijana katika Halmashauri zote nchini. Naomba nitumie nafasi hii kuwaelekeza washirikiane na Maafisa wa Ugani kwenye Wizara ya Kilimo waende wakatoe mafunzo kwa vijana hawa na kimsingi hata ziara ambazo Mheshimiwa Waziri anafanya, Manaibu, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi ndio tunaangalia miradi ambayo imeanzishwa na Halmashauri na kukagua ikiwepo ni pamoja na ufugaji wa samaki katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba tupokee ushauri wake tuwasiliane na viongozi wenzetu wa Wizara ya Uvuvi. Tutalifanyia kazi, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Gashaza nimekuona umesimama kule nyuma.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Ngara tumehamasisha vijana wanaosoma vyuo vikuu nchi nzima wanaotoka Wilaya ya Ngara kwa ajili ya kuweka umoja na ushirika na miaka miwili mfululizo wamekuwa wakija kujitolea wakati wa likizo ndefu kufundisha kwenye shule zetu za sekondari na tayari wamesajili shirika lao linaitwa *Mzalendo Education Organisation (MEO).* Serikali iko tayari kuwashika mkono ili kusudi waweze kuendelea kutengeneza mazingira ya ajira kwa vijana wenzao kwa sababu tayari Halmashauri imeshawapatia ekari 10 kwa ajili ya kuanza miradi ya mfano.

Je, Serikali wako tayari kuweza kuwashika mkono ili vijana hawa wawe mfano kwa vijana wenzao nchi nzima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuunganisha vijana katika eneo lake na kuwapa mawazo haya ambayo ni mawazo mema kweli kweli. Ni kweli, tupo tayari na utayari wetu umeshaanza kutekelezwa. Naomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ngara na Afisa Elimu pale waende katika eneo hili wakutane na vikundi hivi vya vijana, wazungumze nao halafu walete maoni ni kitu gani hasa wanataka kusaidiwa ili waweze kufanya kazi hii nzuri ambayo imeanza. Ahsante sana.

**SPIKA:** Tunaelekea Kilimo, Waheshimiwa Wabunge, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare. Mheshimiwa Massare uliza sasa swali lako tafadhali.

Na. 347

**Kilimo Katika Eneo la Mbuga Kuzunguka Mji wa Itigi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Eneo la mbuga linalozunguka Mji wa Itigi linafaa sana kwa kilimo cha mazao mbalimbali kama mahindi, alizeti, choroko na dengu, lakini eneo hili linajaa maji na kufanya kilimo kuwa kigumu. Je, Serikali ipo tayari kusaidia wananchi wanaolima katika eneo hilo kwa kuwajengea mifereji ya kuongoza maji yasiingie mashambani?

**SPIKA:** Majibu ya wananchi wa Itigi, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la mbuga linalozunguka Mji wa Itigi limekuwa likijaa maji pale mvua zinapokuwa juu ya wastani ambapo historia inaonesha kuwa bonde hili lilijaa maji kipindi cha mwaka 1997/1998 wakati wa mvua za Elnino na katika msimu wa 2015/2016 baada ya miaka tisa tangu wakati wa mvua za Elnino mwaka 1997/1998.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalichukua suala la Mheshimiwa Mbunge na itatuma wataalam wa kilimo na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa ajili ya kwenda kufanya utafiti na tathmini ya kina ya maji kujaa kwenye mashamba ya wakulima. Utafiti na tathmini hiyo itakapokamilika tutakuja na mikakati na mapendekezo stahiki yatakayosaidia kutatua changamoto ya kujaa maji mashambani na kuwasaidia wakulima wa eneo la mbuga linalozunguka Mji wa Itigi ili kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni Magharibi, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini pamoja na majibu haya mazuri sana ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Itigi ni eneo ambalo lina mbuga na ardhi ni nzuri na kama ilivyoonesha kwenye historia kwamba Serikali imekiri kweli kwamba, maji huwa yanajaa.

Sasa je, Serikali iko tayari sasa pamoja na kutuma Tume ya Umwagiliaji wataalam hawa waangalie namna iliyo bora ya kuyavuna maji haya ili yaje kuwa msaada wakati wa kiangazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wananchi wa Itigi na maeneo jirani wanalima sana zao la dengu na kwa kuwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko imekuwa haizingatii sana mazao haya ambayo yanapatikana maeneo ambayo ni machache kama Shinyanga na kwetu Itigi na maeneo ya Tabora suala la dengu.

Je, sasa Serikali iko tayari kufanya juhudi za makusudi kusaidia wananchi hawa wanaolima dengu kupata masoko ya uhakika badala ya kupunjwa na walanguzi ambao huwa wanakuja kila mwaka na bei inakwenda chini? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Wazirfi, Kilimo, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, kwa kifupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anataka kujua kwamba, Serikali kama iko tayari kutuma wataalam wake kwa ajili ya kwenda kufanya tathmini ya kina kule.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo tayari na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba kupitia swali lako hili, natoa maelekezo kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Kanda ya Dodoma kwenda haraka iwezekanavyo katika hii mbuga ya Itigi ili kwenda kufanya tathmini ya kina ili tuone namna gani bora ya kuweza kuvuna maji haya ya mvua yanayosababisha hasara kubwa kwenye hili bonde kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anataka kujua Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Ni kweli Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa mujibu wa sheria ambayo tumeikabidhi kusimamia mazao zaidi ya 35 ikiwemo zao la alizeti na kwamba Serikali tupo tayari kama ulivyoona sasa hivi tupo katika majadiliano ya kina na wenzetu wa India na Vietnam ambao ni wanunuzi wakubwa kwa ajili ya kuingia mkataba maalum wa kuuza mazao haya ya mikundekunde kwa sababu wao ndiyo walaji wakubwa ili tusije kuhangaika na soko huko baadae.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwa sababu wenzetu wameweka *ban* kwenye suala hili la kuingiza kiasi cha dengu na mazao haya ya mikundekunde, sasa tunataka tuingie makubaliano hayo ili tutengeneze soko la uhakika na la bei nzuri kwa wakulima wetu.

Na. 348

**Ulipaji wa Fidia Wananchi wa Wilaya ya Longido na Monduli**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA (K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa ulipwaji fidia kwa wananchi zaidi ya 2,000 wa Wilaya ya Longido na Monduli ambao maeneo yao yalipitiwa na Mradi wa Umeme Vijijini *(REA)?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini inatekeleza mradi wa kupelea umeme katika vijiji vyote nchini ifikapo mwezi Juni, 2021. Lengo la mpango huu ni kuhakikisha kuwa Watanzania zaidi ya asilimia 85 wanatumia umeme ifikapo mwaka 2025. Ili kuhakikisha lengo hili linafikiwa, Serikali inagharamia miundombinu, ujenzi na gharama ya kufikisha huduma hii ya umeme kwa wananchi kwa asilimia 100 na wananchi kulipa shilingi 27,000 tu ikiwa ni Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ya huduma hiyo. Hivyo, miradi ya umeme vijijini haina fidia.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwaomba wananchi wa Longido, Monduli na Watanzania wengine kutoa ushirikiano katika utekelezaji mradi huu ikiwa ni pamoja na kutodai fidia, nakushukuru.

**SPIKA:** Msidai fidia, Mheshimiwa Lolesia.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Serikali imesema kwamba hakuna fidia katika miradi hii ya umeme wa *REA*. Ningependa kujua sasa kwamba je, Serikali ipo tayari kuwaelimisha wananchi kujua kwamba hakuna fidia kabla miradi ile haijaanza kutekelezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna vijiji vingi sana hapa Tanzania ambavyo vimepitiwa na nguzo juu lakini umeme haujashuka kwenye vijiji vile na katika nchi yetu ya Tanzania pia hata katika Jimbo langu limeshuhudia kuna vijiji mpaka sasa mradi wa umeme ulipita tangu mwaka 2014, nguzo zimepita juu lakini wananchi hawajashushiwa umeme.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuangalia vijiji hivyo vyote Tanzania nzima na kuhakikisha kwamba vijiji hivi vinapatiwa umeme vikiwemo vile vya Jimbo la Busanda ambavyo vipo vingi Nyaruyeye na Busaka hawajapata umeme? Niombe Serikali iweze kunijibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Subira Mgalu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Lolesia kwa kazi nzuri anayoifanya lakini maswali yake amejielekeza kwenye namna gani Serikali itaelimisha wananchi. Nichukue fursa hii kwanza kuwashukuru Watanzania wote kwa maeneo mbalimbali ambapo miradi hii ya *REA* inatekelezeka, kwa kweli Serikali, *REA,TANESCO* hata na Wizara yenyewe ya Nishati haijapata changamoto kubwa ya madai ya fidia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwanza Watanzania wenyewe wapo tayari, lakini sisi tutaendelea kuelimisha kadiri tutavyopata fursa kwenye ziara mbalimbali za Mikoa na Wilaya ikiwemo kwenye Jimbo lake la Busanda kwamba wananchi kwa kweli kwa kuwa Serikali inalipia gharama zote na wao wanalipia *VAT* tu shilingi 27,000 na haijawahi kuwa kikwazo, tutaendelea kutekeleza mradi huu na tunawaomba watupe nafasi zaidi na waiunge mkono Serikali yetu ya Awamu ya Tano yenye

nia ya kuhakikisha ifikapo mwaka 2021 vijiji vyote 12,268 vinapata umeme.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameuliza katika vijiji ambavyo vimepitiwa na umeme wa msongo mkubwa lakini havijashushiwa umeme, nikiri kweli tatizo hilo lipo na hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Nishati alivyofanya ziara katika maeneo mbalimbali ya hapa Dodoma, maeneo ambayo miundombinu ya umeme mkubwa imepita lakini hawajashushiwa, wametoa maelekezo kwa *TANESCO* kwamba ifikapo Desemba 2019 maeneo yote yaliyopitiwa na miundombinu ya umeme haijashushwa umeme, ishushwe kwa sababu katika maeneo hayo kinachofanyika ni ujenzi wa line ndogo *LV* na kuweka transfoma na kuwaunganishia wananchi umeme kwa bei ileile ya shilingi 27,000. Kwa hiyo, nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge ikiwemo vijiji alivyota kwenye Jimbo lake la Busanda, Mkoa wa Geita na mikoa mingine yote nchini kwamba tatizo hilo kwa kweli tunaliona na tumeshaliwekea mikakati kama miradi ya *Quiq Wins* katika kupelekea utekeezaji wa mradi huo. Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Nilikuona Mbunge wa Longido swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza kwenye Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, sisi katika Wilaya ya Longido na hata Monduli pia, tumepitiwa na umeme wa msongo mkubwa na napenda kuishukuru Serikali kwa sababu wameshalipa fidia kwa watu wale ambao walistahili kufidiwa, lakini pia naomba kuuliza kwa sababu vijiji vilivyopitiwa katika Wilaya yangu ya Longido ni vitano; Eorendeke, Kimokorwa, Oromomba, Ranchi na Engikaret kuna maeneo mahsusi ambayo jamii iliyatenga kama maeneo ya wazi wakitarajia kwamba fidia yake itakwenda kurudishwa ndani ya kijiji waweze kufanyia miradi ya maendeleo kama kujenga shule, zahanati na kuboresha miundombinu mbalimbali ambayo ni pungufu sana ikiwa ni pamoja na barabara katika vijiji vile.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Wizara itarejesha hizo fedha za maeneo ambayo jamii iliyatenga kama maeneo ya wazi kwa vijiji husika au halmashauri ili tuweze kufanyia hayo maendeleo ambayo tayari wananchi wameshabainisha? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi, Naibu Waziri wa Nishati Mheshimiwa Subira Mgalu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa na nimpongeze kwa kufuatilia masuala ya nishati hususan fidia ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli maeneo aliyoyataja ikiwemo Wilaya ya Longido yamepitiwa na njia ya msongo wa *KV* 400 kutoka Singida – Namanga na tumeshalipa fidia takribani kama shilingi bilioni 44 na maeneo aliyosema ambayo yalikuwa ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za jamii, thamani yake ya fidia ni kama shilingi bilioni 10, utaratibu unaendelea wa kuweza kuyalipa katika maeneo mbalimbali ili pesa hizo ziweze kuchangia shughuli za maendeleo, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana bado tupo Wizara ya Nishati swali la Mheshimiwa Mbunge wa Singida Kaskazini Mheshimiwa Justin Joseph Monko. Mheshimiwa Mbunge wa Singida Kaskazini uliza swali lako.

Na. 349

**Miradi ya Umeme wa *REA* na *BTIP* – Singida Kaskazini**

**MHE. JUSTIN J. MONKO** aliuliza:-

Jimbo la Singida Kaskazini limepata Mradi wa Umeme Vijiji *(REA* na *BTIP)* ambapo utapeleka umeme katika vijiji 54 kati ya 84; katika baadhi ya maeneo ambayo mradi umepita umeacha nyumba za wananchi, taasisi za dini, taasisi za Serikali na pampu za maji pasipo kuziunganishia umeme.

(a) Je, Serikali ina kauli gani kwa maeneo hayo yaliyorukwa na wananchi waliokwishafanya *wiring* kwa matarajio ya kuunanishiwa umeme?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vijiji 30 vilivyosalia?

(c) Je, Serikali ipo tayari kusaidia njia mbadala ya umeme wa jua *(solar power)* katika maeneo ya huduma muhimu kama zahanati, sekondari na huduma za maji wakati tukisubiri usambazaji katika vijiji vilivyosalia?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo bado tupo Wizara ya Nishati, Naibu Waziri Mheshimiwa Subira Mgalu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishaji Vijijini *(REA)* inaendelea kupeleka umeme vijijini kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha umeme katika vijiji, taasisi, viwanda na miradi ya maji na maeneo yaliorukwa katika Jimbo la Singida Kaskazini zikiwemo nyumba za wananchi, taasisi za dini, taasisi za Serikali na pampu za maji zitapelekewa umeme kupitia mradi wa *REA III* mzunguko wa kwanza unaoendelea na kupitia Mradi wa *Densification II* utakaoanza kutekelezwa mwezi Juni, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2020.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme vijijini ambapo vijiji 30 vilivyosalia katika Jimbo hilo vitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili wa mradi wa *REA III* utakaoanza kutekelezwa kuanzia mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

(c) Mheshimiwa Spika, mwaka 2018/2019 Serikali kupitia Mradi wa *Results Based Finance* unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* iliendelea kufanya utafiti ya kujua kiasi cha nguvu ya jua kinachopatikana nchini ikiwa ni pamoja na eneo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa utafiti huo Serikali itaanza kazi ya kupeleka miundombinu ya umeme wa nguvu za jua katika Jimbo la Singida Kaskazini. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Justin Monko swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, awali napenda tu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri aliyefanya ziara yake tarehe 16 Mei ambayo imesaidia sana hasa kwenye Mradi wa *REA III.*

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mgori ambayo ina shule ya kidato cha tano na sita pamoja na Kituo cha Afya cha Mgori pamoja mgodi wa dhahabu pekee tulionao Jimboni wa Mpitipi katika Kata ya Mudida ambavyo vyote vipo katika umeme *wa REA II* havijapata umeme hadi sasa. Mgodi huu upo kilometa tatu tu kutoka ulipo umeme wa *REA* mpaka sasa.

Je, Waziri anawaambia nini wananchi kwamba maeneo haya yatapatiwa umeme lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili Kata ya Kinyeto yenye Kijiji cha Kinyeto, Mkimbii, Ntunduu na Minyaa pamoja na Kata ya Muhama yenye Kijiji cha Muhama na Msikii vipo katika umeme wa *backbone.* Vijiji hivi havijapata umeme mpaka sasa kwa sababu wanahitaji ku-*upgrade* kutoka umeme wa kilovolti 11 kwenda kwenye kilovolti 33.

Je, Mheshimiwa Waziri anatuahidi ni lini zoezi hili la *upgrade* litafanyika ili wananchi hawa waweze kupata umeme, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati majibu ya ufafanuzi kuhusu maswali hayo mawili tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Monko na nimshukuru na yeye na kumpongeza sana kwa kazi nzuri na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Nishati alifanya ziara katika Mkoa wa Singida tarehe 16 Mei na kutoa msukumo mpya wa kasi ya miradi hii.

Mheshimiwa Spika, maswali yake mawili yalijielekeza kwanza kwenye Kata ya Mgori ambayo ipo chini ya *REA II* ambapo kwa kweli kulikuwa na changamoto katika Mkoa wa Singida na Kilimanjaro na ndiyo maana Serikali ilichukua hatua za haraka za kusitisha mkataba na kumpa mkandarasi mwingine na mpaka sasa hivi kazi zinazoendelea katika mradi wa *REA II* wa mkandarasi *EMEC* ni vijiji vinne vimeshawashwa kati ya 16.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo haya aliyoyataja yakiwemo na Mgori na kwenye mgodi huo kwa kuwa kazi inaendelea na kulikuwa na changamoto ya vifaa, Mheshimiwa Waziri aliielekeza *REA* iwasilishe vifaa mapema. Nimthibitishie tu kwa kipindi ambacho tunaelekea mpaka mwezi wa tisa, vijiji 12 vilivyosalia ikiwemo vya Kata ya Mgori vitapata umeme kutokana na jitihada zake za usimamizi na kufuatilia.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameulizia suala la Kata ya Kinyeto ambapo ipo katika mradi wa *backbone* na katika Jimbo hili, mradi huu unahusisha vijiji tisa na mpaka sasa hivi vijiji sita vimeshawashwa bado vijiji vitatu ambavyo Mheshimiwa Mbunge ndiyo ameviulizia hapa. Na kwa kuwa tatizo ni ku-*upgrade* tu kutoka *KV* 11 mpaka 33, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mara baada ya kutoka hapa tufanye

mawasiliano na *REA* na kwa kuwa siyo changamoto kubwa na transfoma za aina hii zipo, ni kwamba ndani ya mwezi tu mmoja mpaka mwisho wa mwezi wa sita huu vijiji vilivyosalia ni vitatu na viwake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nimekuona Mheshimiwa Zedi uliza swali lako.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, tatizo la miradi hii ya *REA* ambapo unakuta mradi umefika kwenye eneo kama kijiji lakini unakuta nyumba, taasisi za kidini, taasisi kama shule, zahanati, pampu za maji zimeachwa bila kuunganishiwa umeme, ni tatizo ambalo lipo pia Jimboni kwangu Bukene na Wilaya ya Nzega yote.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachotaka kujua ni kwamba pamoja na kwamba Waziri alifanya ziara na akatoa maelekezo maalum kwa Mkandarasi wa Wilaya ya Nzega ambaye ni *POMI Engineering* kuhakikisha maeneo yaliyoachwa yanaunganishwa, lakini mpaka sasa mkandarasi huyu inaonekana ameshindwa kabisa kupata vifaa vya kuunganishia maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa nilitaka kujua je, Serikali iko tayari kutoa maelekezo maalum au kumsaidia huyu mkandarasi ili aweze kupata hivi vifaa; waya, nguzo ambavyo inaelekea kabisa kumpata...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:**...ili aweze kufanya kazi ya kuunganisha maeneo hayo yaliyoachwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya swali hilo, wakandarasi hawana vifaa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zedi, Mbunge wa Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze pia Mheshimiwa Zedi kwa kazi nzuri ndani ya Jimbo lake, wiki moja iliyopita tulikuwa katika ziara ya Jimbo lake na nilifanya pia ziara katika Wilaya ya Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umelisema kwa jumla pia suala hili la vifaa, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Zedi na Wabunge wote, kweli zipo changamoto za hapa na pale kuhusu vifaa, lakini tukitathmini mchango wa sekta ya nishati kwenye viwanda vya ndani, kwa sababu changamoto hii imejitokeza baada ya kutoa agizo vifaa vyote vinavyotumika katika mradi huu vizalishwe ndani ya nchi na agizo hili limesababisha kuwezesha viwanda zaidi ya tisa vipya vinavyozalisha nguzo, viwanda zaidi ya vinne vya mita na viwanda zaidi ya vitano vya waya havikuwepo nchini, vyote hivi vimetokana na agizo la kuhakikisha kwamba vifaa vyote vinavyotumika kwenye miradi hii vizalishwe ndani ya nchi ili vilete ajira lakini pia mapato kwa wananchi lakini pia mapato kwa wanaoajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Zedi mimi nikuthibitishie tu sisi kama Wizara tunaendelea kusimamia kuhakikisha changamoto hii inapungua na kama nilivyosema katika majibu mbalimbali ndani ya Bunge lako tukufu, imeendelea kupungua na ndiyo maana leo tunajivunia zaidi ya vijiji 1,400 tumeshaviwasha kwenye *REA III* mzunguko wa kwanza ukiacha na awamu zingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe wito kwa wakandarasi pamoja na ma-*supplier* kwa kuwa wanategemeana, wakae pamoja ili kuondoa vikwazo mbalimbali ambavyo vinaonesha kwamba vinachangia kutokuwepo kwa vifaa kwa wakati katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe tu Wabunge muendelee kutuunga mkono katika hili ili mradi huu

unaotumia shilingi trilioni moja na bilioni 200 uchangie uchumi wa taifa kwa kutekeleza Sera ya Viwanda, asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Wizar aya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali linaulizwa na Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha.

Na. 350

**Mizigo Inaypaswa Kulipa Ushuru Bandarini**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Kumekuwa na kero kubwa sana kwa abiria wanaotumia bandari kwenda Zanzibar kwa boti ambapo hulipishwa ushuru wa bandari kwa mizigo hata boksi la kilo kumi tu au mchele kilo 20 kwa malipo ya shilingi 9,750.

Je, ni mizigo gani ambayo abiria anapaswa kulipia ushiri huo wa bandari *(Wharfage)?*

**SPIKA:** Majibu ya swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kufuatana na mwongozo wa tozo *(tariff book)* kifungu kifungu 29 wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA),* tozo ya *wharfage* inatozwa inatozwa kwa mizigo ya biashara yenye uzito zaidi ya kilo 21 na yenye zaidi ya mita moja ya ujazo inayopita kwenye gati, jeti na maboya yaliyo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA).*

Mheshimiwa Spika, *TPA* haikusanyi tozo yoyote kwa abiria ambao wana vifurushi binafsi *(personal effects)* vyenye uzito au ujazo mdogo chini ya kilo 21 au mita moja ya ujazo wanaotumia bandari kwenda Zanzibar kwa boti kwenye eneo la *baggage room.* Aidha, abiria wanaotumia bandari kwenda Zanzibar kwa boti ambao hutozwa ushuru wa bandari katika eneo la *baggage room* ni wale tu wanaokuwa na mizigo mikubwa tena kwa madhumuni ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika*, TPA* inapenda kuwasisitiza wateja/ abiria wote wenye mizigo ya kibiashara kwenda au kutoka Zanzibar kutumia eneo la *Azam Sea Link* lililotengwa kwa ajili ya shughuli za kibiashara ili kuondokana na usumbufu kwenye eneo la *baggage room* ambalo limetengwa mahsusi kwa ajili ya abiria wenye mizigo yao binafsi *(personal effects).*

Mheshimiwa Spika, tunapenda kutoa wito kwa wateja wetu wote wanaotumia bandari kwenda Zanzibar kwa boti wahakikishe kuwa mizigo yao inapimwa kabla ya kupakiwa ili wajue kama uzito wake unastahiki kutozwa ushuru wa bandari au la, kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, utakubaliana na mimi kwa sababu na wewe pia ni mdau wa Zanzibar, unalea chama chako kwa upande wa Kaskazini na upande wa Kusini na mara nyingi unatumia usafiri wa bandari, hutumii usafiri wa ndege na unakutana na wapigakura.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo bandarini ni kuwa hata kilokumi zinakuwa *charged* na imekuwa ni malalamiko sana kwa wananchi. Ni vigezo gani ambavyo vinatumika kwa mizigo ya biashara na mizigo binafsi kwa hawa wasafiri? Naomba Serikali ifafanue kwa sababu mtu anapita na kilo 20 za mchele anakuwa *charged. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukilalamika mara kwa mara abiria wanaokwenda Zanzibar. Kuna hizi boti za Bakhresa wana nauli zao kwenye mizigo, lakini sasa pale kwenye bandari imekuwa mara kwa mara inarudiana. Naomba kauli ya Serikali, hizi kauli zinazotolewa humu Bungeni ni lini zitafanyiwa kazi kwa vitendo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri lalamiko hili limekuwa kubwa sana pale bandarini kuhusu mizigo ya wanaosafiri kwenda Zanzibar.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, vigezo vinavyotumika nimevitaja na vinapatikana kwenye *tariff book.* Labda hata baadae Mheshimiwa Mbunge naweza pia nikamuelekeza kwa sababu pia *tariff book* iko kwenye *website* ya Mamlaka ya Bandari ili kuweza kuongeza ufahamu na atusaidie kupunguza pia usumbufu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hapa inaonekana kwamba ni uelewa na mimi nitumie tu nafasi hii kutoa maelekezo kwa Mamlaka ya Bandari ili kwamba tuweze kuweka ufafanuzi wa kutosha kwa abiria wanaotumia bandari hii kwenda Zanzibar ili waweze kuweka mabango yanayoonekana kuonesha vigezo vinavyotakiwa huu uzito wa kilo 21 na kwenda mbele ndiyo wanatakiwa kutozwa. Lakini pia waweze kutoa ufafanuzi na kutoa maelekezo na mimi ntalifuatilia hili ili kuona kwamba hili tunalitekeleza kupunguza usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo nia ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuona wananchi wake wanateseka.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo ndiyo maana nasema nitafuatilia ili kuona kwamba usumbufu unaondoka, uelewa unaongezeka kwa wananchi wanaotumia bandari. Wakati mwingine wanaingia kwenye kutozwa kutokana na kutokuelewa.

Mheshimiwa Spika, lakini msisitizo mkubwa niseme tu kwamba wale wanaofanya biashara wapitie kwenye eneo maalum kama nilivyosema, ambalo ni kwa ajili ya biashara, wakijichanganya na abiria wengine inaongeza usumbufu ambao Mheshimiwa Mbunge ameutaja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, amezungumza kwamba kuna usumbufu kwenye usafiri wa boti ya Bakhresa, na wiki iliyopita tu kulikuwa na swali lilijibiwa hapa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Serikali tutaendelea kuchukua hatua na tutafuatilia vizuri ili menejimenti ya mamlaka iweke usimamizi madhubuti ili wananchi hawa wasiendelee kupata shida na sisi kama viongozi upande wa Wizara tutalisimamia hili ili usumbufu tuweze kuupunguza na hatimaye tuumalize kabisa.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, lakini tumshauri tu Waziri, kama kweli kilo 21 ndiyo *most minimum* kwenye boti ipo haja ya kuangalia. Kilo 20 hata sanduku la mwanafunzi tu yaani linazidi, hata baadhi ya mashirika ya ndege yanatoa kilo zaidi kidogo ya 20, sasa kwenye boti kilo 20 kidogo sana. Kwa hiyo, iko haja ya kuangalia, kama siyo sheria ni kanuni tu, hata ukibeba mihogo mitatu tu kilo 20 ilishavuka. Kwa hiyo hilo ni la kuliangalia. Wanaokwenda na kutoka Zanzibar angalau wapate raha kidogo. Hii kero ya wananchi imekuwa kubwa, muiangalie Serikali. *(Makofi)*

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo tafadhali.

Na. 351

**Kutoa Matibabu Bure kwa Wagonjwa wa Sickle Cell**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Mtoto mwenye ugonjwa wa *sickle cell* hutakiwa kupata matibabu mfululizo ambapo kwa familia zisizo na

uwezo hushindwa kulipia gharama za matibabu na hivyo kusababisha mgonjwa kupoteza maisha.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wagonjwa wa *sickle cell* kupata matibabu bure?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa watoto wenye ugonjwa seli mundu au kwa jina la kitaalam *sickle cell,* wanahitaji matibabu mfululizo kwani huwa wanapata upungufu wa damu na maumivu ya mara kwa mara. Familia, jamii na wadau mbalimbali wamekuwa wakijitahidi sana kuwahudumia watoto hao kwa kuwapatia mahitaji maalum. Hata hivyo, misaada hiyo haikidhi mahitaji ya wagonjwa wote na kuna baadhi ya familia hazina uwezo wa kuwahudumia watoto wenye seli mundu.

Mheshimiwa Spika, kwa kulitambua hilo, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeandaa mwongozo wa kutoa msamaha kwa makundi tofauti yasiyo na uwezo likiwepo kundi la watu wenye magonjwa sugu kama *sickle cell.* Kwa kupitia Maafisa Ustawi wa Jamii, familia zisizo na uwezo huhakikiwa na kupatiwa kibali cha huduma bila malipo. Aidha, Serikali inaanzisha Mpango wa Taifa wa Udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza *(National Non-Communicable Diseases Control Programme)* ambayo ugonjwa wa *sickle cell* utakuwa ni moja ya magonjwa yatakayokuwa yakiratibiwa kitaifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Restituta swali la nyongeza, swali muhimu kuhusu wagonjwa wa *sickle cell.*

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa ugonjwa wa *sickle cell* unatokana na mtoto kurithi *cells* kutoka kwa baba na mama yake, wazazi wake wote wawili wanakuwa na *cells* ambazo ziko *half.* Sasa mtoto anapozaliwa anakuwa amerithi zile *cells* ndiyo maana anazaliwa na huo ugonjwa.

Je, ili kuzuia hili tatizo Serikali ina mkakati gani wa kuwapima watoto wanapozaliwa kwenye vituo vya afya na katika hospitalini mara tu wanapozaliwa iwapime ili wagundulike kwamba wana ugonjwa wa *sickle cell* ili kuepusha vifo vya watoto kwa sababu mara nyingi wanapogundulika wanakuwa wameshakuwa watu wazima na wengi huwa wanapoteza maisha, hasa vijijini?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa *commitment* kwamba Serikali inaandaa mwongozo wa kutoa msamaha wa matibabu bure kwa familia ambazo hazijiwezi kupitia kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii, sasa basi, yako magonjwa kama UKIMWI na *TB* watu hawahakikiwi, wanapata matibabu bure.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa bure matibabu ya *sickle cell* bila kuhakikiwa kama ilivyo magonjwa ya UKIMWI na *TB?*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Restituta Mbogo kwa kuwa ni mfuatiliaji wa karibu wa magonjwa haya yasiyoambukiza na hususani ugonjwa huu wa seli mundu.

Mheshimiwa Spika, hoja yake inahusiana na suala la upimaji wa watoto wanapozaliwa. Ni kweli ugonjwa huu huja

kwa njia ya pale wazazi wanapokuwa na vinasaba ambavyo vinahamishwa katika kipindi cha ujauzito kuja kwa watoto pale wazazi wanapokuwa na vinasaba hivi vya ugonjwa huu wa seli mundu, *genetic transfer.* Kwa hiyo, katika nchi ambazo zimeendelea, watoto ambao wana Ugonjwa huu wa seli mundu wanaweza wakabainika kwa njia mbili; njia ya kwanza ni kupima ujauzito wakati mtoto akiwa bado tumboni kwa kupitia katika maji yaliyopo katika mfuko wa uzazi, unaweza ukabaini kwamba mtoto anaweza akazaliwa na ugonjwa wa seli mundu. Lakini njia ya pili, baada ya mtoto kuzaliwa akipimwa anaweza akabainika kama ana ugonjwa huu wa seli mundu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi; Tanzania na nchi nyingi za Afrika ugonjwa huu ni mkubwa na wako wagonjwa wengi na sisi kama Serikali, pamoja na kazi nzuri ambayo imefanyika pale Hospitali ya Muhimbili kupitia programu ile ambayo inaongozwa na madaktari mahiri ya Profesa Julie Makani, wamekuwa wanatoa msaada mkubwa sana kwa wagonjwa hawa wa seli mundu. Sasa sisi kama Serikali tumeamua sasa tunataka tuje na mpango wa kitaifa ambao utasimamia matibabu haya ya seli mundu na ndiyo maana tumesema kwamba ifikapo Novemba programu hii tutakuwa tumeianzisha rasmi na mkakati wa upimaji unaweza ukawa ni moja ya mkakati huo ambao tutaweza kuufanya kuhakikisha kwamba tunaubaini ugonjwa huu katika hatua za awali na kuweza kuwatibu hawa wagonjwa vizuri zaidi na kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linahusiana na suala la uhakiki wa wagonjwa. Ili uweze kumbaini mgonjwa wa seli mundu ni lazima kwanza apimwe na kuthibitishwa. Katika utaratibu ambao tunao sasa hivi hizo njia ambazo nimezisema hapo awali hatuzifanyi, kwa hiyo, mara nyingi unakuta mgonjwa anakwenda akiwa na tatizo la upungufu wa damu au akiwa na zile *crisses,* maumivu makali ambayo anayapata kutokana na ugonjwa huu, na akishathibitika kwamba ni mgonjwa wa *sickle cell* anapata matibabu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa hatuna mfumo wa matibabu bure kwa wagonjwa wa seli mundu na hili niseme tu kwamba pale anapobainika mgonjwa kwamba hawezi kugharamia matibabu, kwa utaratibu wa sasa tuna utaratibu wa misamaha na utaratibu ni ule ambao nimeusema katika jibu langu la msingi, wanatakiwa kupita katika Serikali zao za Mtaa au Serikali za Vijiji kupata barua, wakija kwa Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi ya hospitali watapata matibabu bure. Lakini katika mpango ambao tunataka kuanzisha mwezi Novemba tutaweka utaratibu mzuri zaidi wa matibabu kwa wagonjwa hawa wa seli mundu.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na Wizara ya Maliasili naomba tusikilizane. Waheshimiwa Wabunge tafadhali, maana yake wengine yaani kama vile hatuko pamoja kabisa, wana yao. Naomba tusikilizane kidogo Waheshimiwa Wabunge.

Ninaye mgeni maalum kwenye *gallery* ya Spika ambaye ninapenda kumtambulisha mapema. Naye ni Spika wa Bunge la Rwanda, anaitwa Donatille Mukabalisa, Mheshimiwa Spika wa Rwanda, ahsante sana na amesindikizwa pale na Naibu Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia, nakushukuru sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Spika wa Rwanda amefuatana na Balozi wa Rwanda nchini Tanzania Eugene Kayihura, karibu sana. Lakini pia amefuatana na Mbunge ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Siasa na Jinsia, Rubagumya Emma, ahsante. *(Makofi)*

Lakini pia na Mbunge mwingine, ni Mwenyekiti wa Masuala ya Hesabu za Serikali Ngabitsinze Chrysostome; karibu sana na amefuatana na Mwambata wa Ubalozi wa Rwanda nchini Tanzania, Ndugu John Kizito. *(Makofi)*

Lakini pia Spika amefuatana na wasaidizi wake watatu, Ndugu Nzabonimana Serge. Lakini pia amefuatana

na walinzi wawili; Nkubito Dieudonee ambaye yeye ni Meja wa Jeshi na msaidizi mwingine wa Spika ni Luteni Gatete Oswald, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, Spika huyu amekuwa Mbunge tokea mwaka 2000 kwenye Bunge la Rwanda. Pia amewahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi na Biashara kwenye Bunge lile, amewahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Siasa, ni Spika kwa kipindi cha pili, kwa mara ya kwanza alichaguliwa mwaka 2013. *(Makofi)*

Tofauti na hapa kwetu, ni kwamba Spika wa Rwanda kwa Katiba yao anatoka katika chama tofauti na chama tawala. Kwa hiyo, yeye ni kiongozi wa chama kinachoitwa *Liberal Party.* Lakini niseme hapa hapa, Rwanda hawana vyama vya upinzani, yaani hawana vyama vile vya kupinga kila kitu kama hapa, ni kweli, yaani ndiyo *facts,* wao wana vyama vya ushindani, kuna *difference* kubwa hapo, wana vyama vya ushindani. Kile cha kupinga tu haiwezekani. *(Makofi)*

Historia yake amewahi kuwa Mhadhiri wa Sheria katika Chuo Kikuu cha Rwanda, lakini pia amewahi kufanya kazi zaidi ya miaka 16 katika Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo *WHO* na *UNDP.*

Waheshimiwa Wabunge, na wao wana Mabunge mawili; wana Bunge la *Senate* na lile Bunge kama la kwetu hili ambalo wanaita *Chamber of Deputies* ambalo ndiyo lina majukumu kama haya ya kwetu. Taratibu zao za kazi za Kibunge kule Rwanda ni kwamba Kamati huwa zinakutana asubuhi, saa tatu hadi saa sita mchana, halafu Bunge lenyewe linaanza saa sita hadi saa 12 jioni, ndiyo utaratibu wanaoutumia na wanakutana mwaka mzima. *(Makofi)*

Lakini pia Bunge la Rwanda ndilo lenye rekodi ya kuwa na Wabunge wengi wanawake duniani. Jumla ya Wabunge wao ni 80 na kati ya hao 80, 54 ni wanawake ambayo inafikia asilimia 68. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunamkaribisha sana Mheshimiwa Spika, Donatille Mukabalisa. Kama mnavyokumbuka Waheshimiwa Wabunge wengi mmewahi kutembelea Rwanda, mmepokelewa vizuri sana na mlipata kila aina ya ushirikiano. Kwa niaba yenu namshukuru sana Spika, na wao nao wametutembelea safari hii. Basi ni vizuri mkafahamu kwamba tuna ugeni huu na wale wote ambao mtakuwa katika ratiba ya kukutana na Mheshimiwa Spika tufanye hivyo na pia atapata nafasi ya kukutana na Wabunge wote wanawake katika kikao maalum, ratiba mtapewa na utaratibu mtapewa.

Tunaendelea na Maliasili na Utalii, swali la Mheshimiwa Zubeda Sakuru.

Na. 352

**Ongezeko la Matumizi ya Kuni na Mkaa**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA (K.n.y. MHE. ZUBEDA H. SAKURU)** aliuliza:-

Ongezeko la gharama za nishati nchini hasa umeme na gesi vimesababisha kuwa na ongezeko kubwa la matumizi ya kuni na mkaa.

Je, ni lini Serikali itarasimisha biashara ya mkaa ili kupunguza makali ya maisha hasa kwa Watanzania wenye kipato duni?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, biashara ya kuni na mkaa inafanyika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Misitu pamoja na Tangazo la Serikali Na. 324 la tarehe 14 Agosti, 2016 na Mwongozo wa Uvunaji wa Mazao ya Misitu wa mwaka 2007 uliofanyiwa marekebisho mwaka 2015. Hivyo biashara hii ni rasmi na haina kizuizi chochote kwa mwananchi yeyote, kinachotakiwa ni kufuata sheria na taratibu za kufanya biashara ambazo zimefafanuliwa vyema katika mwongozo wa uvunaji ambao unamtaka kila mvunaji wa miti kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa kuzifuata, kitu ambacho baadhi ya wafanyabiashara na wachoma mkaa hawatimizi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya taratibu hizi ni pamoja na:-

(i) Kutambua na kutenga maeneo ya misitu kwa ajili ya kutengeneza mkaa.

(ii) Kila anayehusika na shughuli za biashara ya mkaa anatakiwa kusajiliwa na Meneja wa Misitu wa Wilaya na anatakiwa kuwa na leseni.

(iii) Maombi ya usajili na leseni yanapaswa kupelekwa kwa Afisa Misitu wa Wilaya na kujadiliwa na Kamati ya Kusimamia Uvunaji wa Wilaya; na

(iv) Kila mfanyabiashara wa mkaa anapaswa kulipia mrahaba kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 14 la Sheria ya Misitu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba mkubwa wa nishati ya miti, Serikali inawahamasisha Watanzania na wadau wote kuanzisha mashamba ya miti kwa ajili ya matumizi ya nishati.

Hata hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge kuisaidia Sekta ya Misitu kwa kuhamasisha matumizi ya umeme, gesi, uzalishaji wa nishati mbadala ili kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na mkaa ambayo inaongeza uharibifu wa misitu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja kama una swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na mkanganyiko wa matamko kutoka kwa Wakala wa Misitu nchini kwamba mtu akipatikana na kilo 50 za mkaa ni lazima awe na kibali maalum; ni marufuku kwa mtu kupatikana na kilo 200 za mkaa na adhabu yake ni kifungo cha miezi kumi au kulipa faini ya shilingi 50,000 na shilingi milioni 12. Hivi ni sahihi kabisa watu kama akina mama lishe, mama ntilie, akina mama wa nyumbani, adhabu hii inawahusu?

Mheshimiwa Spika, katika swali langu la pili kwa kuwa gesi siyo ajenda tena kwa Serikali hii ya wanyonge na mtungi wa gesi hivi sasa kilo 15 ni kati ya shilingi 45,000 mpaka shilingi 50,000; hivi ni kwa nini Serikali isione kuna umuhimu wa kuondoa kodi katika gesi ili kuwawezesha wananchi waweze kutumia gesi badala ya kutumia mkaa na kuni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii Mheshimiwa Constantine Kanyasu tafadhali

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Devotha Minja, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninakiri kwamba limekuwepo tamko kutoka ofisini kwetu linalohusiana na namna tunavyojipanga kudhibiti ukataji na uchomaji hovyo wa mkaa na tumeelekeza kwamba wahusika wa biashara ya mkaa ambao wanafanya biashara, siyo watumiaji, wahusika wa biashara ya mkaa ambao wanasafirisha mkaa kwa ajili ya kuuza wanapaswa kuwa wamepitia taratibu mbalimbali kabla ya kuchoma mkaa na taratibu hizo zinaanza katika *level* ya vijiji, tunaowazungumzia hapa siyo watumiaji wa mwisho kwa maana ya mama lishe na

watumiaji wa ndani hawa watakwenda kununua katika maeneo maalum ambayo tumeelekeza maeneo yote yanayofanya biashara ya mkaa yatasajiliwa na wale wanaofanya biashara ya mkaa pale ndiyo watakaowauzia watumiaji wa mwisho.

Kwa hiyo, ni makosa kuwakamata watumiaji wa mkaa wa ndani ambao wamenunua kwa muuzaji ambaye ametambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kweli kwamba gharama ya gesi iko juu na hii imesababisha watu wengi ku-*opt* kutumia mkaa na kuni hasa maeneo ya vijijini, lakini watafiti wanaonesha kwamba bado kwa gharama ya sasa matumizi ya gesi ni gharama nafuu kuliko matumizi ya mkaa. Kwa mfano sasa hivi gunia la kilo 50 la mkaa katika Jiji la Dar es Salaam linauzwa mpaka shilingi 60,000 wakati mtungi wa gesi unauzwa shilingi 50,000 na muda wa matumizi ya gesi ni muda mrefu kuliko matumizi ya mkaa.

Mheshimiwa Spika, lakini nimechukua mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge na tutajadiliana na Wizara husika kuona kama tunaweza tukaomba kuondolewa kwa baadhi ya kodi kwenye gesi ili kuhamasisha matumizi ya gesi na kupunguza matumizi kuni. *(Makofi)*

**SPIKA:**Ahsante sana, tunahamia Wizara ya Maji Waheshimiwa Wabunge swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi.

Na. 353

**Serikali Kuchimba Visima vya Maji – Vijiji vya Jimbo la Lulindi**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Wananchi wengi wa Vijiji vya Mieji, Utimbe, Naliongolo, Mtolya, Geuza na Mchoti wamekuwa wakiliwa na mamba na wengine kujeruhiwa vibaya hasa

wanapokwenda kuchota maji katika Mto Ruvuma kutokana na ukosefu wa maji katika maeneo yao.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kuchimba visima vya maji katika vijiji hivyo ili kunusuru wananchi wanaouawa na kujeruhiwa na mambo wnapofuata maji katika mto huo?

**SPIKA:**Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi Mbunge wa Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wa vijiji vya Miesi, Utimbe, Naliongolo, Mtolya, Geuza na Mchoti wana shida ya kupata majisafi na salama na sehemu pekee ya kupata maji ya matumizi ya nyumbani ni kutoka Mto Ruvuma. Hata hivyo kutokana na umbali uliopo kati ya vijiji hivyo inapelekea gharama ya kuchukua maji katika Mto Ruvuma kuwa kubwa ukilinganisha na gharama ya kuchimba visima.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ya Masasi inategemea kuingia mkataba wa kuchimba visima na Wakala wa uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa *(DDCA)* katika vijiji 26 kwa gharama ya shilingi milioni 579.

Mheshimiwa Spika, rasimu ya Mkataba wa uchimbaji wa visima katika vijiji 26 umewasilishwa Wizarani na tayari kibali kimetolewa kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo.

**SPIKA:**Ahsante sana Mheshimiwa Bwanausi swali la nyongeza.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ninatambua kazi nzuri inayofanywa na Waziri na Naibu Waziri katika Wizara hii. Ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali langu la kwanza, je, kwa kuwa vijiji vya Nairombo, Nanjota, Msanga ni vijiji ambavyo vinapitiwa karibu na bomba kuu la Mradi wa Chiwambo pamoja na Mradi wa Shaurimoyo ikiwa ni pamoja na Kijiji cha Nakachindu. Je, Serikali ipo tayari sasa wananchi hawa ambao wako karibu na bomba kuu waweze kupatiwa maji?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ni kwamba tunao mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma ambao unakaribia kukamilika wenye thamani ya shilingi bilioni 3.6 na mradi huu wakati ukiandaliwa kijiji cha Chipingu ambacho kipo karibu na mradi kilikuwa hakina umeme wa *REA* na sasa pale pana umeme wa *REA.*

Je, Wizara ipo tayari sasa kupeleka umeme kwenye mradi huu ambao ni kilometa mbili ili wananchi waweze kupata maji kwa urahisi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya katika Jimbo lake lakini kwa kuwa mfatiliaji wa mara kwa mara Wizarani katika kuhakikisha suala la maji linatatuka katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo hususan kwa vijiji ambavyo vipo karibu na bomba kuu kupatiwa maji na tumefanya mageuzi makubwa sana katika Wizara yetu ya Maji. Moja ya mageuzi hayo ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote ambavyo vinapitiwa

na bomba kuu kilometa 12 katika upande wote wa bomba kuu vinapatiwa maji.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama viongozi wa Wizara hatutokuwa kikwazo katika kuhakikisha vijiji vile ambavyo vipo karibu na bomba kuu vipatiwe maji. Lakini kuhusu suala zima la mradi ule wa maji kupatiwa umeme wa *REA* nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafanya mawasiliano na Mhandisi wa Maji atuletee *document* na sisi kama viongozi wa Wizara ili tuweze kuwezesha mradi ule uweze kutekelezeka wa *REA,* ahsante sana.

**SPIKA:**Ahsante sana swali la nyongeza nimpe Mheshimiwa Mbunge anayetoka karibu kabisa na Rwanda, Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa mradi wa vijiji 56 unaoendelea kule Kyerwa usanifu umekamilika. Sasa swali kuna kata ambazo zina hali ngumu sana kama Kata ya Bugomola, Kata ya Kibale, Kata ya Businde na Kata ya Bugala.

Je, Serikali wakati tunaendelea kusubiria huu mradi uanze wako tayari kuwachimbia wananchi visima ili waweze kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru lakini nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya nataka nimuhakikishie sisi tupo tayari na tunalishukuru Bunge lako tukufu limetuidhinishia sisi Wizara ya Maji zaidi ya shilingi bilioni 610 katika kuhakikisha tunatekeleza miradi ya maji bila shaka tutampa nafasi hiyo katika kuhakikisha tunamsaidia visima.

**SPIKA:**Ahsante sana. Swali la mwisho kwa siku ya leo la Mheshimiwa Mbunge wa Igalula Mheshimiwa Musa Ntimizi tafadhali

Na. 354

**Jimbo la Igalula Kupata Maji toka Ziwa Victoria**

**MHE. MUSA R. NTIMIZI** aliuliza:-

Serikali ina mpango wa kuleta maji katika Mkoa wa Tabora toka Ziwa Victoria lakini Jimbo la Igalula halipo katika ratiba hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vijiji vya Jimbo la Igalula katika mradi huo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hilo la watu wa Tabora na Igalula kw aujumla. Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Tabora, Igunga na Nzega pamoja na vijiji zaidi ya 80 vilivyopo umbali wa kilometa 12 kila upande kutoka bomba kuu. Vijiji vilivyopo katika Jimbo la Igalula vipo umbali wa zaidi ya kilometa 30 toka linapopita bomba kuu, hivyo kushindwa kuingizwa kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imeanza kutekeleza miradi mbalimbali katika Jimbo la Igalula kwa kutumia vyanzo vya maji vingine ambapo kwa sasa usanifu unaendelea katika Kata za Tura, Nsololo na Loya. Ujenzi wa miradi hii, inategemewa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:**Mheshimiwa Ntimizi tafadhali.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwanza kabisa kwa masikitiko makubwa napenda kupokea majibu yasiyoleta matumaini ya kupata maji kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Igalula.

Mheshimiwa Spika, Waziri ni shahidi, amekuja Jimboni kwangu na Mheshimiwa Makamu wa Rais tulizungumzia kero hii ya maji, alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu na alikuja Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kwamba maji ya Ziwa Victoria yatakuja katika Jimbo la Igalula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Jimbo la Igalula vijiji vyake viko zaidi ya kilometa 30 linapopita bomba la maji, lakini naomba nikwambie linapojengwa tenki kubwa linalopeleka maji Sikonge na Urambo ambapo ni takribani kilometa 100 na zaidi liko kilometa 18 toka Jimboni kwangu. Lakini wananchi wa Jimbo la Igalula hawapati maji ya ziwa Victoria.

Mheshimiwa Waziri ajiweke katika nafasi yangu aone namna gani tabu napata Majimbo yote ya Mkoa wa Tabora yanapata maji ya Ziwa Victoria kasoro Jimbo la Igalula tu. Lakini ndani yake kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais. Je, Wizara itatekeleza lini ahadi hii ya Mheshimiwa Rais? La kwanza. *(Makofi)*

Lakini la pili amezungumzia miradi ya Tura, Nsololo na Loya ambayo usanifu wake umeshafanyika muda mrefu na *documents* zimeshafika Wizarani muda mrefu lakini haipo katika *financial year* 2018/2019 pamoja na shida kubwa ya maji tuliyokuwa nayo katika Jimbo la Igalula. Je, Waziri ananiambia nini na wananchi wa Jimbo la Igalula leo wanasikia wanataka kusikia kauli ya Waziri? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu majibu Mheshimiwa Naibu Waziri unapeleka maji kwa Mama Sitta, wapi kila mahali Igalula hupeleki maji kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwanza nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kiukweli sisi kwa Mkoa wa Tabora tumeona ni eneo ambalo limekuwa na changamoto kubwa sana na ndiyo maana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ametupa zaidi ya shilingi bilioni 600 katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji katika Mkoa wa Tabora kuyatoa maji Shinyanga na kuyapeleka katika Mkoa wa Tabora, lakini kupeleka mpaka Kaliua pamoja na Urambo kwa Mama yetu Sitta.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge subira yavuta heri. Tumeanza utekelezaji wa awamu ya kwanza na hatuna kikwazo chochote, nataka nimuhakikishie baada ya maji kufika Tabora tutamhakikishia kwamba tunayapeleka katika eneo lile na ahadi ni deni, tutahakikisha tunatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kumtua mwanamama ndoo kichwani.

Lakini kuhusu suala zima la kibali kuhusu suala la utekelezaji ama usanifu wa Loya, Mheshimiwa Mbunge nataka nimhakikishie naomba baada ya saa saba tukutane na wataalam wetu ili hili jambo tulifanye kwa haraka ili wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:**Mheshimiwa Keissy nilikuona.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa maji Kirando Mheshimiwa Naibu Waziri anaujua, Waziri anaujua. Je, lini sasa mtampa mkandarasi kazi aanze kupeleka maji katika Kijiji cha Kirando wakati tumeokoa huo mradi shilingi bilioni tatu ilikuwa shilingi bilioni 7.5 tukawabana majizi na wengine waka fukuzwa kazi kwenda usanifu wa pili mradi umefika shilingi bilioni 4.6 lakini mpaka leo hajapewa mtu mwenye uwezo kwenda kumalizia ule Mradi wa Maji Kirando?

**SPIKA:**Kirando majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kiukweli amefanya kazi kubwa sana na sisi kama viongozi wa Wizara tumefika katika eneo lile la Kirando kiukweli moja ya miradi ambayo imekuwa ikichezewa ilikuwa miradi ya maji vijijini na tunalishukuru Bunge lako tukufu na Mheshimiwa Rais itakapofika tarehe 1 Julai miradi yote ambayo imekuwa ikisimamiwa na Halmashauri inarudi kwetu katika Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie makandarasi kwa maana ya Kampuni pamoja na Wahandisi wa Maji ambao wametutia hatiani sisi Wizara ya Maji hawana nafasi ya kazi katika Wizara yetu ya Maji. Lakini makampuni yale mengine yote tutayafutia na katika kuhakikisha kwamba hayatofanya kazi yoyote katika Wizara yetu ya Maji, na nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya kutatua changamoto ile na kuokoa fedha tunamuagiza mkandarasi kwa maana ya utangazaji wa kazi ili ianze mara moja ili wananchi wake wa Kirando waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana

**SPIKA:**Mheshimiwa Juma Nkamia nilikuona swali la mwisho kabisa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Farkwa walishafanyiwa tathmini wananchi wa Mwambose na Bubutole na sasa hivi hawaruhusiwi kuendeleza makazi yao wala kuzika watu wanaofariki wanakwenda kuwazika porini.

Naomba kauli ya Serikali ujenzi wa bwawa hili upo? Kama haupo wawaambie wananchi wale ili waweze kuendeleza makazi yao.

**SPIKA:**Ahsante sana majibu ya swali hilo, Farkwa ipo au haipo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mkubwa sana katika kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya maji na maslahi yao mengine.

Mheshimiwa Spika, tunaona kabisa katika mji huu wa Dodoma kumekuwa na ongezeko kubwa na Serikali imehamia, kuna haja sasa ya kuongeza wazalishaji wa maji. Serikali imeona haja sasa ya kuanzisha hili Bwawa la Farkwa katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji Dodoma pamoja na eneo lake la Chemba.

Mheshimiwa Spika, tumekwishafanya usanifu lakini sasa hivi tupo katika hatua ya utafutaji fedha katika kuhakikisha kwamba tunawalipa wananchi fidia na utekelezaji wa mradi ule. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mradi ule upo na sisi kama Serikali tupo mbioni katika utafutaji wa fedha katika kuhakikisha tunawalipa wananchi fidia na utekelezaji uanze mara moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:**Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge maswali yetu ya leo yameisha, tuishie hapo tuna wageni kama mtakavyoona *gallery* zetu zimejaa kabisa nitawaomba tupitie pitie.

Lakini kwanza niwapongeze Waheshimiwa Wabunge maana yake mmerudi kwa kishindo kutoka kwenye mapumziko, sikutarajia mahudhurio makubwa kiasi hiki siku ya kwanza inaonyesha huko wapiga kura ni wakali na nimepata *message* nyingi sana yaani kila *message* inakumbushia kumbushia vipi mabaki mabaki hakuna huko? Wabunge wangu wako hoi, sikukuu ndivyo ilivyo sikukuu ya Eid ni sikukuu kubwa, kwa hiyo lazima mambo yaende vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, niwatangazieni kwamba *TWPG* inawatangazia Wabunge wote wanawake kwamba leo tarehe 10 Juni, saa 10 jioni Spika wa Bunge la Rwanda Mheshimiwa Mukabalisa Donatille atakutana na wajumbe

wa kamati ya utendaji ya *TWPG* Kamati ya Utendaji *TWPG* saa 10.00 kamili jioni ukumbi wa Spika mtakuwa na kikao, Kamati ya Utendaji.

Lakini leo leo saa 12.30 jioni Spika Mukabalisa kwa chakula cha jioni pale *Morena Hotel* atakutana na Wabunge wote wanawake. Wabunge wote wanawake saa 12.30 jioni *Morena Hotel* kwa chakula cha jioni. Naomba nisisitize saa 12.30 jioni ikifika muda na mambo yanaanza. Kwa hiyo, siyo 12.30 jionindiyo unaanza kutoka kwako hapana. Kwa hiyo nawaombeni sana akinamama wote 12.30 jioni *Morena Hotel.*

Nina wageni 20 nafikiri watakuwa *somewhere* kule juu wanatoka Sekondari ya Namnyaki iliyoko Imagi, Kilolo. Wasichana wa Namnyaki simameni, ahsante sana. Hawa mabinti..., endeleeni kusimama hawa warembo hawa ni mabinti kutoka katika jamii ya Kimasai ambao walikuwa *previously* wamelazimishwa kuolewa kwa nguvu wakiwa bado hawajafikia umri huo, wakaamua wao kuitafuta elimu chini ya Mkurugenzi wao Bwana Edward, kwa hiyo, wamekwenda kule Kilolo wamepata elimu na wanaendelea vizuri na elimu.

Kwa hiyo, Dkt. Kiruswa na wenzako hii mila bwana hii, *TWPG* bebeni hii maneno hii, kaeni na Wabunge wa maeneo yote hayo muone ni mbinu gani tunaweza kutumia kuokoa maisha, si mnaona mabinti hawa jinsi ambavyo sasa wangekuwa wanafanya mambo mengine kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kuja nadhani kama Mheshimiwa Mwamoto kama hawaondoki kama wako mpaka leo jioni na wenyewe waende kwenye *dinner* ya Mama Sitta ya *Morena Hotel* kwa mwaliko wa Spika eeh muende *Morena Hotel* kama mtakuwa hamuondoki pia jioni mpate *dinner* pamoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ni wageni kutoka Shirika la Ndege la *Precision Air* ambapo leo tuna Mwenyekiti wa *Precision Air* Ndugu Michael Shirima. Mzee

Shirima ni mjasiriamali ambaye ndiyo wana-*run Precision Air* tunakupongeza sana kwamba mtanzania na Watanzania wenzako mnaweza kusimama na kuendesha Shirika la Ndege, hongera sana tunakutia moyo sana na tunaona ndege za *Precision Air* zikija hapa Dodoma na kutoa huduma vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

Mzee Shirima amefuatana na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa *Precision Air* Patrick Mwanri karibu sana na Meneja Mauzo - Najma Ndassiwa. Meneja Mauzo Ndassiwa ahsante huyo hapo na Meneja Mkoa wa Dodoma - Mercy Isinika karibu sana na Meneja Mauzo Mkoa wa Dodoma - Ndugu Devota Feruzi, ahsanteni sana. Wananiambia hapa *Precision Air* imejipanga kutoa *first class service* kwa Waheshimiwa Wabunge wakati wowote mnapohitaji kusafiri. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Ndugu Fonth Alex mmiliki wa Kampuni ya Kings Chocolate ya Ubelgiji na mnunuzi wa kokoa Kyela, Busokelo na Rungwe, karibu sana. *(Makofi)*

Huyu anashughulika na *chocolate* kule Ubelgiji na zinatokana na kokoa inayolimwa kule Kyela. Lakini pia mamefuatana ya watu wawili maofisa kutoka kampuni Bayolands ambao ni wanunuzi wa kokoa Ndugu Emmanuel Mwacha na Mdugu Frank Samwel, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga - Waziri wa Kilimo ambao ni wapiga kura wake kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe ambao Ndugu Fadhali Fwambo. Ndugu Faraji Omari na Ndugu Moses Madenge, karibu sana kutoka vwawa popote pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Angellah Kairuki - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji kutoka Wilaya ya Same Mkoa wa Kilimanjaro. Oooh karibu sana, karibu sana wageni wetu kutoka kule Same, *jakaya,* ahsante sana wanasema *chedi. (Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa - Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni wana *jogger* wenzake kutoka *Muungano Jogging and Sports Club* ya Mkoani Dodoma. *Muungano Joggers,* hao hapo karibu sana na Mheshimiwa atakuwa kule mahali anarekebisha mambo ili akirudi hapa awe kamili kamili. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Doto Biteko Waziri wa Madini ambao ni jamaa zake kutoka Singida Mjini Ndugu Dura Sumbaye na Ndugu Martin Kahuka, wale kule. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Andrew Chenge kutoka Halmashauri ya Bariadi, Mkoa wa Simiyu ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri wa Mji wa Bariadi Ndugu Robert Mgata na Mtumishi wa Halmashauri wa Mji wa Bariadi Ndugu Lina Kilumbi hao apo karibu sana. (*Makofi*)

Wageni 98 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza, lakini nitawatambulisha kwa makundi; kundi la kwanza ni wanafunzi waliomaliza kidato cha nne mwaka 2018 Shule ya Sekondari ya *Sunshine,* Kibaha Pwani na kupata *division one* na *two* wapo 39 wakiongonzwa na Mkuu wa Shule hiyo Ndugu Frank Raphael wale wa *Sunshine,* aaaah wale kule karibu sana. Hawa wamemaliza *form four* mwaka jana na wamepata *division one* na *two* toka *Sunshine,* ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu kuna waliomaliza darasa la saba mwaka 2018 shule ya msingi *St. Anne Marie Academy,* Dar es Salaam kwenye Wilaya hii shule ya Anne Marie ilikuwa ni ya kwanza kwenye Mkoa wa Dar es Salaam ni ya kwanza na kitaifa ilikuwa ni shule sita, jumla ya wageni hawa wapo 59 wanaongozwa na Makamu Mkuu wa Shule Ndugu Amos Joseph. *(Makofi)*

Wale wa Anne Marie ahsante sana na hongereni sana hii imekuwa shule ya msingi wa kwanza na hongera sana Mheshimiwa Jasson Rweikiza unaimarisha elimu hongera sana. Haya ndio mambo Wabunge tunatakiwa tufanye, sio Mbunge unamiliki Noah unamtia aibu Spika kila siku unaonekana *traffic* huko unamiliki bodaboda Mbunge,

tuvuke jamani mambo haya. Bodaboda zikikamatwa unampigia Spika bodaboda zangu zimekamatwa huku sasa inakuwa..., tuvuke kidogo Waheshimiwa Wabunge. *(Kicheko)*

Wageni 50 wa Mheshimiwa Halima Bulembo ambao ni Wajumbe wa Baraza la Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Kagera. Wajumbe wa Baraza kutoka Mkoa wa Kagera hongereni sana na karibu sana vijana wa Chama cha Mapinduzi Kagera naamini kabisa mmejipanga huko Kagera au sio? Safi sana yupo Mheshimiwa Selasini anawaona. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari ya Kisaba iliyopo Lushoto, Mkoani Tanga. Wale wa Kisaba, hongereni sana. Hawa Kisaba katika hiyo *form four* iliyomaliza mwaka jana wanafunzi 25 wamekwenda kidato cha tano na wanafunzi 19 wameenda vyuo mbalimbali, hongereni sana na hii ni sekondari ya kata. Wale waliokuwa wanadharau shule zetu za kata wanaona matokea jinsi yalivyo mazuri. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Hussein Bashe ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Nzega, Mkoa wa Tabora. *UDOM* kutoka Nzega, eeeh hata wanyamwezi mnasoma vyuo vikuu siku hizi! Hongereni sana na karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Yosepher Komba ambao ni viongozi wa CHADEMA kutoka Wilaya ya Muheza, Mkoa wa Tanga wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama hicho wa Wilaya Ndugu Josephat Swai, wale kule kwani hicho chama bado kipo? Karibu sana kutoka Muheza, watani zetu hawa siku moja moja lazima tuwastue kidogo. *(Kicheko)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Pascal Haonga, ambao ni wanachama wa CHADEMA kutoka Mbozi, Mkoa wa Mbeya karibu sana, karibu sana siku nyingine mje wengi kidogo sasa watano wangapi mje kidogo100. *(Makofi)*

Wageni 12 kutoka Taasisi ya *Hope Delivery Foundation* ya Jijini Dodoma karibu sana Hope, tunafurahi kuwaona kwa mara nyingine Hope karibu sana na kama mtakuwa na programu zozote basi tutaonana baadaye kidogo, lakini karibu sana muwe pamoja na Waheshimiwa Wabunge namtupatie elimu katika mambo ambayo mngependa kufahamu zaidi karibu sana *Hope*. *(Makofi)*

Wanafunzi 24 na walimu sita kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana Loreto ya Jijini Mwanza wakiongozwa na Mwalimu Innoncent Ezekia wale kule hongereni sana na karibu sana Loreto. *(Makofi)*

Idara ya Utawala inawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba zoezi la kujiorodhesha kwa ajili ya kupata idadi kamili ya Waheshimiwa Wabunge watakaoshiriki katika zoezi la kulenga shabaha katika Kambi ya Jeshi ya Makutupora litahitimishwa siku ya Jumatano (kesho kutwa) tarehe 12 Juni. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge ambao bado mnajiorodhesha na mnahitaji kushiriki zoezi hilo bado linaendelea muende pale kwenye dawati la mapokezi pale utawala mjiandikishe ili wafanye taratibu za usafi na maandalizi mengine.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua timu yetu ya Taifa imeshatangulia Misri kwa ajili ya maandalizi ya mashindano la *AFCON* ya mwaka huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ngereja - Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazieni na kuwaombeni..., Waheshimiwa Wabunge tusikilizane tunaombwa kwa wale Wabunge ambao tunapenda kwenda kushuhudia Fainali za Kombe la Afrika *(AFCON)* nchini Misri mwaka huu, tuendelee kujiandikisha kupitia Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa John Kadutu, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Cosato Chumi. Tujiandikieshe kwa wale ambao tungependa kwenda, utaratibu mzima wa safari umeshatolewa kupitia mitandao yetu ya Kibunge. Gharama za safari unachangua mwenyewe kama unataka kwenda awamu zote mbili au awamu moja au awamu ya pili.

Lakini awamu ya kwanza ambayo ni siku nne ni dola 720 tu *comprehensive*, usafiri pamoja na mambo mengine pamoja na ukiwa Misri kupelekwa uwanjani na kurudi hotelini. Awamu ya pili ni siku sita hii gharama yake ni dola 770 tu. Kwa hiyo, ukitaka kwenda safari zote mbili ni kama dola 1400 hivi unaweza ukaa siku zote hizi nne na hizi sita zikawa siku 10.

Kwa hiyo, *at list* mojawapo Waheshimiwa Wabunge tukashiriki, tujiandikishe kwa hawa wenzetu mapema na tuweze kulipia mapema ili kuhakikisha kwamba tunafanya *booking* za uhakika, tuweze kwenda kuiona timu yetu ikifanya mambo yake kule Misri na wale wa awamu ya kwanza kama wale wa siku nne chache zile na mimi nitalipia nitaenda, kwa hiyo, kwa wale wa awamu ya kwanza tunaweza tukawa pamoja. *(Makofi)*

Tunaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuuonge mkono timu yetu ni miaka mingi sana hatujafika *AFCON*. Kwa hiyo, wachezaji wakicheza wakiwa wanaona Wabunge wametoka hapa kwenda kuwaunga mkono naamini itawapa nguvu kuwa zaidi.

Naamini Mheshimiwa Waziri wa Michezo baadae kidogo hata kama sio leo atatupatia tena maelezo ya ziada ya kuhusiana na masuala haya mashindano haya ya *AFCON*. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Waheshimiwa Wabunge kulikuwa ni michezo katika *weekend* hii juzi na jana ambapo *Bunge Sport Club* walitoka suluhu pamoja na *Mwanza Veteran* kwenye mpira wa miguu, lakini kwenye mpira wa pete Bunge waliwafunga *Mwanza Veteran* 27 kwa 17. *(Makofi)*

Jana Jumapili palikuwa na bonaza la michezo ambapo *Bunge Sport Club* waliwafunga *Rwehikiza Heroes* mbili kwa moja na baadae *Bunge Sports Club* wakaendelea kucheza tena *Vodacom* ya Dodoma na *Bunge Sports Club* ikashinda kwa bao moja kwa bila. Tunawapongeza sana *Bunge Sports Club* kwa ushindi huo wa michezo ya aina mbalimbali. *(Makofi)*

Baada ya hapa kama mnavyujua ratiba yetu ni ya Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi kukutana kwa majadiliano na Serikali, Kamati hizo zitakutana saa ngapi tutawasiliana. Tutakutana leo lakini tutawasiliana baada ya mawasiliano na Serikali, kuna *consultation* zinahitaji zifanyike naamini itakuwa mchana. Lakini tutapeana taarifa baadae kidogo kwamba ni saa ngapi tunakutana na tunakutana katika ukumbi wetu wa kawaida wa Msekwa ule ambao unaweza uka-*accommodate* Kamati mbili.

Basi baada ya hapo shughuli za mezani kwa siku yaleo zimekamilika. Kesho kutwa siku ya Alhamisi ni siku ya Bajeti tarehe 13 Juni kama kawaida kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kujianda kwa ajili ya kupokea Bajeti ya Serikali siku hiyo.

*Otherwise* shughuli za hapa mezani zimekamilika na kwa jinsi hiyo basi naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 4.33 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 11 Juni, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*